
# ACHA WAFU WAWAZIKE WAFU WAO



JAMES KALEKWA

# ACHA WAFU WAWAZIKE WAFU WAO:

*Wito mchungu, wenye hatima tamu.*

James Kalekwa

# Orodha ya yaliyomo

Kusoma Biblia: ........ 4

Kuhusu "Kufa/Wafu" ........ 6

Fundisho potofu la maziko. ........ 8

Kipaumbele cha urithi wa mali ........ 10

Maana ya usemi huo mkali ni nini? ........ 11

Injili inapohubiriwa, wafu wanafufuka ........ 13

Maswali ya kujihoji ........ 15

1. Je, Yesu ni Bwana na Mwokozi wako? ........ 15
2. Je, Yesu amewaambia wengine habari za wokovu wa Yesu? ........ 16
3. Je, Yesu anakuita kumtumikia? ........ 18

Kuhusu Mwandishi: ........ 19

Kuhusu New Vine Church: ........ 19

Mawasiliano na Mwandishi: ........ 20

“21. Mwingine katika wanafunzi wake akamwambia, Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu

22. Lakini Yesu akamwambia, Nifuate; waache wafu wawazike wafu wao.”

**Mathayo 8:22**

“59. Akamwambia mwingine, nifuate. Akasema, Bwana, nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu.

60. Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu.”

**Luka 9:59-60**

## Kusoma Biblia:

Ili kujenga uelewa mpana wa Biblia ni vizuri kuelewa mambo kadhaa:

i. Muktadha (context) wa mazungumzo
ii. Utamaduni wa watu wanaohusika kwenye mazungumzo hayo
iii. Zama/Wakati wa mazungumzo husika
iv. Tafsiri pana (implication ya mazungumzo)

Maandiko yaliyorejelewa hapo awali ni mazungumzo baina ya Yesu na mtu mmoja ambaye aliitwa na Yesu awe mfuasi (atumike kwenye Ufalme), lakini yule ndugu akatoa sababu kwanini hatamfuata Yesu kwa wakati huo. Alisema anapaswa kwenda kumzika baba yake mzazi!

Kwenye utamaduni wa Kiyahudi kuzika ilikuwa ni zaidi ya tukio la kulaza mtu kaburini, bali ilimaanisha mambo yafuatayo: Mosi, ulikuwa ni wajibu wa mzaliwa wa kwanza kukaa na babaye hasa baba anapokuwa anaelekea siku za mwisho wa maisha yake (anakaribia kufa) – ama kwa ugonjwa au umri kusogea sana. Hali hii ya kukaa karibu na baba alikuwa ni ishara ya upendo na wajibu wa mtoto kwa mzazi lakini pia ndio ulitoa uhalali (legitimacy) kwa mtoto kupokea baraka za mzaliwa wa kwanza (kupokea maradufu ya kile alichomiliki mzazi wako). Kwahiyo, kukaa na baba mpaka afikwe na mauti ilifahamika kama **“kumzika baba”.**

Pili, kwenye utamaduni wa Kiyahudi baada ya baba (mtu yeyote) kufariki dunia na kuwekwa kaburini (kuzikwa) aliachwa kwa siku 7 ili mwili uvimbe na kupasuka, baada ya hatua hii ya kwanza ya msiba *"shivah",* zilifuata siku 30 za maombolezo zilizojulikana kama "shloshim". Hata hivyo msiba na maombolezo huendelea mpaka pale ambapo mwili ulioza na kutoweka na kubakiza mifupa tu (inakadiriwa kuwa muda takribani miezi 12 *"ossilegium"*). Kwahiyo, mtoto alipaswa kukaa hali ya kuomboleza na kusubiri muda fulani, mathalani mwaka mmoja ili baada ya hapo achukue mifupa na kuizika tena (reburry). Hii ilikuwa na tafsiri ya kimapokeo ya kwamba mwili uliooza na kubakisha mifupa ni ishara ya kwamba marehemu amevuka hukumu na amepokelewa mbinguni *(kama vile fundisho la pagatory).*

Siku hii ya kuhamisha mifupa ilikuwa ni siku ya furaha sana kwa ndugu hasa watoto wa marehemu… Ilikuwa ndiyo siku ya kuanua matanga – kufikia mwisho wa maombolezo.

## Kuhusu "Kufa/Wafu"

Kuna dhana kadhaa za kifo kwenye neno la Mungu. Kuna kifo ambacho kinafamika kwa haraka na wengi,

yaani roho ya mwanadamu kutengana na mwili wake kama yanenanvyo maandiko matakatifu.

*"Na mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa."*
**Mhubiri 12:7**

Lakini pia dhana ya kifo kwenye Biblia imetumika kuashiria mambo mengi…
Ukirejelea Warumi 7:4 (SUV) Maandiko Mtakatifu hunena hivi:
*"Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda."*
Ninataka uone hili neno ***"kufia torati"*** na pia ukisoma Warumi 6:11 (SUV) neno la Kristo husema:
*"Vivyo hivyo nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu."*
Haoa nimekusudia uone neno ***"wafu kwa dhambi"***

Utagundua dhana ya kifo imetumika kumaanisha athari ya jambo kwenye maisha ya mtu; yaani, ni kwa namna gani maisha ya mtu huyu yanaguswa na kuendeshwa na jambo linalotajwa. Kwa kiingereza hutumiak neno *"influence"…* Uwezo wa kitu husika kuyaathiri maisha ya mtu binafsi. Kwahiyo, unapokuwa mfu kwa habari ya dhambi au torati

maana yake vitu hivyo havina nguvu tena kuyaathiri/kuyaongoza maisha yako binafsi.

Sasa turudi kwenye habari yetu ya msingi kuhusu wafu kuwazika wafu wao; Yesu alijibu kwa mkazo namna hiyo si kwa kuwa alikuwa hapendi watu au hapendi ndugu washughulikie mambo ya ndugu zao hasa maswala ya maziko. Yesu anapenda watu kiasi kwamba Yeye mwenyewe aliwafufua wafu kadhaa na kuponya wagonjwa. Yesu alikuwa na huruma kwa watu kwa kutazama hali zao, uhitaji na mazingira yao.

*“Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”*

**Mathayo 9:36**

Pia, Yesu anasisitiza juu ya maswala yahusianayo na familia mathalani swala la kuwaheshimu wazazi!

“Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako.”

**Mathayo 19:19**

## Fundisho potofu la maziko.

Mkazo wa Yesu, *“Waache wafu wawazike wafu wao…”* ulikuwa ni kukinzana na lile fundisho la kimapokeo la maombolezo endelevu ya takribani mwaka mmoja

ambayo huhitimishwa na kuzika mara ya pili (reburrying). Kulikuwa na mapokeo ya kimaziko ambayo yalikuwa yanaendelea wakati huo. Kulikuwa na maziko ya mara ya kwanza ya mwili na kulikuwa na maziko ya mara ya pili ya masalia ya mwili – ambayo ilikuwa na maana fulani.

Ifahamike ya kwamba maziko ya mara ya pili (baada ya mwaka mmoja wa maziko ya awali) yalifanyika kwa kukusanya mifupa ya marehemu na kuiweka kwenye kifaa maalum cha kuhifadhia. Hii ilikuwa ni ishara ya kwamba marehemu amevuka hukumuni na kuingia kwenye uzima wa milele pamoja na Mungu (Rejea fundisho la pagatory kwenye historia ya kanisa). Hii si sawasawa… hili si fundisho sahihi hata kidogo!

*"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa ni hukumu"*

***Waebrania 9:27***

Unaweza kurejea habari ya Lazaro (Bwana ni tumaini langu) na tajiri aliyekuwa akila kwa anasa. Hii itakupa kuelewa andiko la Waebrania nililoambatanisha hapo juu. Soma Luka 16:19-31

Kwahiyo Yesu hakutaka kuunga mkono (endorse) fundisho hilo kwa kumpa ruhusa yule ndugu. Yaani, Yesu angemruhusu huyo ndugu kwenda kwenye ibada

ya kimapokeo ya maziko angekuwa anaunga mkono fundisho lililo nyuma ya mapokeo hayo.

## Kipaumbele cha urithi wa mali

Inawezekana ya kwamba baba ya kijana huyu hakuwa amekufa bado (kama nilivyokuonyesha hapo awali). Lakini, alikuwa na umri umesogea au amedhoofika; yuko kwenye masaa ya jioni ya maisha yake. Utamaduni wa wakati huo vilevile ulimaanisha ya kwamba kijana alipaswa kukaa na baba yake aliyekuwa anasubiri kufa. Kwamba atakufa lini? Haijulikani! Wengine walikaa miaka kadhaa ya "masaa ya jioni" ya maisha yao; na kwa sababu hiyo kijana alipaswa kukaa miaka yote hiyo akimsubiri baba yake afariki.

Hata hivyo, nyuma ya kusubiri mauti ya baba itokee, kulikuwa na kusubiri kupokea *"sehemu ya mali inayoniangukia"* (Luka 15:12). Ni kungojea urithi wake. Inawezekana baba yake alikuwa na mali ambazo akizipokea maisha yake yangesogea hatua nyingi kwenda mbele. Kwa hiyo, akaona asicheze mbali. Akae "kumzika" baba yake ili apokee uhakika wa maisha yake!

Kwa upande mwingine, mwito alioitwa na Yesu ungemkosesha urithi toka kwa baba yake. Hii

ilimuweka kijana njiapanda ya vipaumbele. Alitaka na alipenda sana kumfuata Yesu lakini alipenda sana pia kupata urithi. Bwana Yesu alitaka kuhakikisha moyo wake uko sehemu moyo. Siyo moyo uliogawanyika huku na kule.

Kimsingi, Yesu alichokifanya ni kumfunulia kijana yule hali ya moyo wake; maisha yake ya kiroho. Alikuwa amekufa ndiyo maana alikuwa anaenda kuzika wafu!

## Maana ya usemi huo mkali ni nini?

Kuna wanatheolojia husema, huenda Yesu alimaanisha kazi ya kufanya ibada hiyo ya kimapokeo ni ya watu walio katika hali ya kifo cha kiroho (wanaoishi katika ibada za mapokeo). Yaani ni watu ambao kwa muonekano wa nje wako hai lakini ndani wamekufa. Kwahiyo ni wajibu wa wafu wa kiroho kuwazika kimapokeo wafu wao wa kimwili… Sijui unaelewa kitu hapo?

Yaani, si sawasawa ibada hii ya kimapokeo ya kuzika wafu ifanywe na watu walio hai kiroho. Tafsiri hii hujulikana kama *The Majority Interpretation (MI)* miongoni mwa wasomi wa Theolojia.

Tafsiri yake pana ni kwamba, kama lengo la ibada hiyo ni kuwaona watu wakivuka kutoka mautini na kuingia uzimani basi lengo ni sahihi lakini njia si sahihi. Njia pekee ya kuwasaidia watu waingie uzima wa milele si

kusubiri mpaka wafe, na kusubiri tena mwaka mmoja zaidi; bali ni kuwafikia na habari za Ufalme wa Mungu hali wakiwa hai ili wafanye maamuzi… na huu ndiyo wito ambao Yesu alimwitia yule ndugu aliyetaka kwenda kuzika *"wafu"*- baba yake!

Kuna kundi jingine la wanatheolojia husema ya kwamba Yesu alimaanisha ya kwamba kwenye makaburi kuna wafu wengine wanaosubiri kufikisha mwaka mmoja ili mifupa yao izikwe tena, basi hao wanapaswa kuwazika wafu waliofikisha muda wa maziko ya mara ya pili.

Ili kuelewa hili, ni vyema ifahamike ya kwamba hapo kale kwenye jamii za Kiyahudi kila familia, ukoo na jamaa walikuwa na makaburi yao. Maeneo waliyoyatenga maalumu kabisa kwaajili ya maziko. Makaburi hayo yalichongwa kwenye miamba. Hayakuwa ni makaburi ya kuchimba mashimo kama ilivyo kwenye zama zetu. Kwahiyo, ndani ya jengo/mwamba mmoja wa kaburi anaweza kuzikwa zaidi ya mtu mmoja. Ni kwa mantiki hiyo basi ya kwamba, wafu waliomo ndani ya kaburi moja wanaweza kuhudumia kwa habari ya maziko ya mara ya pili – ile ibada ya kimapokeo! Hii itamaanisha ya kwamba wafu wanaosubiri muda watawazika wafu waliotimiliza muda wa kimapokeo… wafu kuwazika wafu wao!

**Hitimisho**

Sehemu bora na sahihi ya kuyahamisha maisha ya watu kutoka kwenye upotevu na kuingia uzimani ni ng'ambo hi ya maisha – watu wakiwa hai. Ukisubiri mpaka wamefikwa na mauti ndiyo ufanye Ibada za kimapokeo ili wahamishwe, huo ni upotofu na upotevu wa muda kwa mujibu wa Bwana Yesu. Kazi ya kupoteza muda kiasi hicho hufanywa na wafu walio hai kwenye maisha haya [kama utaelewa mara moja basi Bwana asifiwe]. Kwa wewe uliye hai ndani ya Kristo Yesu, unapaswa kuwafikia watu wengi iwezekanavyo na kuwaambia habari njema za Bwana Yesu ili waweze kumwamini Yeye na kazi aliyoifanya msalabani. Kwa kufanya hivyo watahakikishiwa uzima wa milele hali wakiwa hai hapa duniani na hivyo utapunguza mwendelezo wa Ibada za wafu kuzika wafu!

## Injili inapohubiriwa, wafu wanafufuka

"Pozeni wagonjwa, **fufueni wafu**, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."

**Mathayo 10:8**

"1. Nanyi **mlikuwa wafu** kwa sababu ya makosa na dhambi zenu

5. Hata wakati ule **tulipokuwa wafu** kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema.

6. **Akatufufua pamoja naye**, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;”

**Waefeso 2:1, 5-6**

Wakati Yesu anatoa maelekezo kwa wanafunzi wake juu ya kuhubiri injili; moja ya jambo ambalo aliliagiza ni kufufua wafu. Kwanza, ina maana hii ambayo inakuijia kichwani. Kuwatoa kwenye hali ya roho kutengana na mwili.

Pia, ni vyema kufahamu kutokea kwenye neno la Mungu ya kwamba kila mtu ambaye hajamwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake kibinafsi ni mfu! Dhambi inamfanya mtu kuwa kwenye hali ya umauti. Na dhambi inayozungumziwa hapa ni kutokumwamini Yesu Kristo.

Mtume Paulo anatufunulia ya kwamba, kila mmoja wetu alikuwa kwenye hali hiyo ya umauti. Kila mmoja wakati fulani alikuwa ni mfu kwasababu ya makosa na dhambi.

Hata hivyo ufufuko unakuja ndani ya mtu pale anapoikubali zawadi ya msamaha wa bure wa Yesu Kristo kwa kumwamini na kumkiri, yaani, kutambua kazi ya msalaba ya Yesu kulipia dhambi zetu.

Nini hutokea injili inapohubiriwa? Muujiza wa kwanza ni watu kumwamini Bwana Yesu na kusamehewa dhambi zao. Yaani, watu kutoka kwenye hali ya mauti kwa sababu ya dhambi; ni watu kuignia kwenye uzima wa milele… watu wanarudi tena kwenye maisha. Wafu wanafufuka!!!

## Maswali ya kujihoji

Kusoma neno la Mungu, kuelewa muktadha na maana na kufanya uchambuzi haitakuletea mabadiliko yoyote kwenye maisha. Ni maandiko yaliyotendewa kazi tu ndiyo huwaletea watu matokeo.

Ninataka kuwasilisha kwako maswali haya ujiulize na uone hatua stahiki ya kuchukua.

### 1. Je, Yesu ni Bwana na Mwokozi wako?

Kama bado hujampokea Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yako, sina maneno mazuri ya kukuambia zaidi ya haya… wewe ni mfu! Unahitaji kupokea uhai leo. Na hapa simaanishi iwapo huwa unaenda kanisani au ibadani au una dini. Je, umemwamini Yesu Kristo?

Kama bado, ninakukaribisha ufanye hivyo leo. Neno linasema:

"9. Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. 10. Kwa

maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."

Warumi 10:9-10

Una hiyo nafasi ya kufanya hivyo leo. Sema maneno haya kwa sauti:

Bwana Yesu, ninatambua ya kwamba mimi ni mwenye dhambi. Na ninatambua ya kwamba Wewe ni Mtakatifu. Na dhambi zangu zimenitenga mbali na Wewe. Sina njia ya kunisaidia kutoka kwenye hali ya dhambi. Ninaomba hivi leo, uniokoe na kuniondoa kwenye hali dhambi. Ninaitambua kazi uliyoifanya msalabani; ninaiamini na kuipokea kwenye maisha yangu. Karibu Yesu uwe Bwana na Mwokozi wangu. Tangu sasa, mimi ni mali yako.

Asante Yesu kwa kunipenda na kuniokoa.

Katika jina la Yesu Kristo nimeomba na kuamini. Amina!

Kwa maombi hayo umeokoka. Hongera kwa kufanya maamuzi ya thamani namna hii.

## 2. Je, Yesu amewaambia wengine habari za wokovu wa Yesu?

Kuna watu wamekuzunguka ambao bado hawajamwamini Yesu; ni wafu! Umezungukwa na maiti. Je, umechukua jukumu la kufufua wafu hao? Yesu alimwambia yule kijana

*"Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu."*

*Luka 9:60*

Tumeokolewa ili tuwafikie wengine waokoke. Hatujaitwa kukaa tu. Tumeitwa kuutangaza ufalme wa Mungu.

Ni rahisi tu na inawezekana.

Tengeneza Orodha ya watu kumi. Ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi wenzako, jirani. Kisha anaza kuwaombea. Halafu pata muda kuwaambia habari za Bwana Yesu.

Ujumbe wa injili ya wokovu ni mkubwa. Lakini pamoja na ukubwa wake ni ujumbe ambao unaelezeka.

a) Waonyeshe ya kwamba wanadamu wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu Rejea: **Warumi 3:23**
b) Waonyeshe ya kwamba dhambi inastahili hukumu ya Mungu **Rejea: 6:23**
c) Waonyeshe ya kwamba Mungu alichagua kutupenda hali tukingali wenye dhambi. Hatukufanya chochote kustahili upendo huo Rejea: **Warumi 5:8**
d) Waonyeshe uchaguzi ni wao kufanya. Ni wao wenyewe wanachagua uzima wa milele unaotolewa na Yesu. Na hapa unaweza ukasema namna wewe binafsi ulivyokutana na

wokovu wa Bwana Yesu Rejea: **Warumi 10:9-10**

e) Kisha waongoze kwenye maombi ya kumkaribisha Bwana Yesu ndani ya mioyo yao kuwa Mwokozi.
f) Baada ya hapo wakaribishe kanisani (unapoenda wewe) ili wakutane na familia kubwa ya imani.

3. Je, Yesu anakuita kumtumikia?

Inawezekana Yesu amekuwa akiweka wito ndani yako wa kutumika kama askari wa mstari wa mbele kwenye huduma. Unaitwa kuwa mmishonari, kwenda kufungua kanisa mahali fulani; unaitwa kufikia jamii fulani kwa injili; unaitwa kuwa Mchungaji; unaitwa kuwafundisha watu neno la Kristo. Na umekuwa ukisubiri mambo yawe sawa.

Acha wafu wawazike wafu wao!

*"Hapo inenwapo, leo, kama mtaisikia sauti yake, Msiifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha."*

**Waebrania 3:15**

Kama umewekewa mwito ndani yako, itika!

Ninashauri upate kusoma kitabu kilichopo kwenye huu mradi wa vitabu 20 vya kieltroniki vya bure kiitwacho **MASUMBUFU YA MAISHA:** *adui mkubwa wa kusikia maelekezo ya Mungu.*

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi  wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja

kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764